**NOVENA YA BIKIRA MARIA MFUNGUA MAFUNDO 03/05/2019 – 11/05/2019**

**SIKU YA KWANZA**
**SALA YA UTANGULIZI**.
Nasadiki kwa Mungu baba Mwenyezi.
Sala ya Imani
Sala ya matumaini
Sala ya Mapendo
Sala ya kutubu

SALA KWA BIKRA MARIA MFUNGUA MAFUNDO
Mama yetu mpole Maria mfungua mafundo,chanzo Cha amani na furaha,unayajua maisha yangu vizuri kwamba yamejaa mafundo ambayo yananifanya nikose hewa Mara kwa mara.Yamenifanya mfungwa na ninaomba ukombozi Kutoka kwako mama.Ninaaminia upendo wako wako wa kimama na ninajua kwamba kwa njia ya maombezi yako kwa mwanao,utayafungua moja baada ya jingine.Nataka kuishi maisha mapya ya mtoto wa Mungu na ninaamini kwamba Bwana hataniacha bali atanipa maisha mapya ya mwili, akili na roho.

Naomba nisiwe peke yangu katika vita hivi vya kiroho bali unielekeze na uniongoze katika bonde hili la machozi.Pamoja nawe kama msafiri mwandamana ninauhakika wa kuwa kwenye njia sahihi.

Fungua mafundo yangu yote leo ninaposubiri muda ule ambamo utafungua fundo la mwisho la maisha yangu nitakapokuwa huru mbali na dhambi zote na nitakapomwona Bwana wetu uso kwa uso katika heri ya milele mbinguni.Amina

**Sali mafungu matatu ya rozari(mafumbo ya siku hisika)**

SOMO LA BIBLIA
*Nitaweka uadui Kati yako na huyo mwanamke,na Kati ya uzao wako na uzao wake,watakuponda kichwa nawe utawaponda kisigino Mwz 3:15*

Ee Maria umejaa neema tangu milele ulichaguliwa kuwa mama wa Mkombozi wetu na mama wa waamini wote.Niheshima gani kubwa kwangu kukuita mama yangu.Mwenye unyenyekevu kama mtoto nawasilisha kwako fundo hili...(taja ombi lako)ambalo limenifanya mfungwa kwa miaka hii yote.Nalikataa.Mama Maria mfungua mafundo,haribu pia mizizi yote ya fundo hili ili leo niweze kuwa mwana wa Mungu aliyefanywa upya.

Ee Maria mama yangu,chukua fundo hili ili lililonifanya mfungwa wa kiroho na kwa neema yako lifungue.

**Maria mfungua mafundo,niombe mimi ninayekukimbilia**
**Sali mafungu mawili ya mwisho ya rozari**

**Sala ya Mwisho ya kila siku**
**Bikra Maria mfungua mafundo.**
Maria mama yetu mfungua mafundo kumbuka you kwamba haijasikika kamwe kuwa aliyekukimbilia akitaka umsaidie ulimwacha bila kusaidiwa.Nikichochewa na matumaini hayo na nikielemewa na dhambi zangu na mateso yangu ninakimbilia ulinzi wako kwa moyo wa majuto Ee mama.Mama wa Neno la Mungu usiakatae maombi yangu lakini unihurumie na usikilize Sala yangu.

Unafungua mafundo yote katika maisha yetu Ule mkanda mrefu wa mafundo unanyooshwa katika mikono yako ya kimama na ya Mapendo Sasa nakuja kwako Ee Bikira wa mabikira,ona mafundo mangapi yananiziba pumzi maisha yangu.Unao a mateso ya maisha tena na tena.
Unaona nilivyopooza.Ee Maria uliyepata neema Imakulata mwenye kufungua mafundo katika maisha ya wanao naweka mikononi mwako marindp haya

-Changamoto za Kiroho
-Changamoto za mahali ninapofanyia kazi
-Changamoto ninazozibeba katika maisha yangu na ambazo hazina ufumbuzi

-Mafundo yaliyosababishwa na tabia yangu, kukosa uvumilivu kukosa uwezo wa kuisikiliza,hasira,wivu,kutaka kulipa kisasi mashindano, woga,chuki,kukosa usalama,kiburi,kutovutiwa na wenzangu,hangaiko la moyo, huzuni,ulafi, kushindwa,na uchoyo.
-Mafundo ya mioyo yetu iliyo migumu inayotuzuia kupenda kwa ukarimu na kusamehe kwa urahisi
-Mafundo yanayosabaishwa na matambiko,mazingaombwe,ushirika, uchawi, kupiga ramli.
-Mafundo kama matokeo ya kutoelewanna katika familia Kati ya wazazi na watoto,matendo ya ukatili na mgawanyiko.
-Mafundo ya kukosa ajira
-Mafundo ya msongo wa moyo kati ya mme na mke
-Mafundo yatokanayo na ulevi wa kupindukia na matumizi ya madawa ya kulevya
-Mafundo ya matokeo ya ugonjwa usiotibika
-Mafundo yanayosababishwa na maumivu Kutoka kwa wengine
-Mafundo yanayosababishwa na kuhukumiwa na dhamiri na utoaji wa Mimba.

Kwa unyenyekevu na kwa UTUKUFU wa Mungu tunakuomba ufungue mafundo haya yasiwepo tena milele.Tunakutumainia kwa kuwa wewe ni faraja yetu pekee Ee mama.Yapeleke yote kwa Yesu mwanao Bwana wetu.Kwa maombezi yako yenye nguvu hakuna fundo hata moja linaloweza kubaki limefungwa.Kwa Imani kubwa tunatamani ulinzi wako wa pekee na wa uhakika maana hakuna aliyekimbilia msaada wako akakataliwa.Maria mfungua mafundo utuombee kwa Mwanao na Bwana wetu sasa na hata milele.Amina.

**SIKU YA PILI**
**Sala ya utangulizi rejea sala ya utangulizi ya siku ya kwanza**
**Sali mafungu matatu ya Rozari**
**(Mafumbo ya siku husika)**

Somo la Biblia
*Mwezi wa sita malaika Gabriel alitumwa na Mungu kwenda mpaka mji wa Galilaya,jina lake Nazareth kwa mwanamwali Bikira aliyekuwa ameposwa na mtu,jina lake Yusufu,wa mbali ya Daudi jina lake Bikira huyo ni Mariam.Akaingia nyumbani kwake akasema, Salamu uliyepewa neema,Bwana yu pamoja nawe(Lk1:26-28)*

Maria, umejaa neema, binti mpendelevu wa Mungu na kwa Imani najua kwamba una nafasi ya pekee Sana mbele za Mungu.Kwa Imani hii naamini pia kwamba Mungu Baba ana nafasi ya pekee kwa ajili yako.Ni uhusiano wa kina Sana,si kwako Maria lakini pia kwa watoto wako wa kiroho Najua kwako Maria nikiweka mikononi mwako na fundo hili......(taja fundo) linalo nitesa na kuniweka mbali na Mungu Baba yangu, Kristo Mkombozi wangu na Roho Mtakatifu uliye wangu mtakasa.Ninaamini kwamba utayafungua ili maisha yangu yaweze kuungana na Utatu Mtakatifu.

**Maria mfungua mafundo,niombee mimi ninayekukimbilia.**
**Sali mafungu mawili ya mwisho ya rozari**
**Sali Sala ya mwisho Sala inapatikana kwenye novena ya siku ya kwanza.**
**Kwa Maria mfungua mafundo**

**SIKU YA TATU**

**Sala ya utangulizi**
**Sali mafungu matatu ya Rozari**
**(Mafumbo ya siku husika)**

Somo la Biblia
*Malaika akamwambia,usiogope,Mariamu kwa maana umepata neema kwa Mungu.Tazama utachukua Mimba na kuzaa mtoto mwanamume;na jina lake utamwita Yesu (Luk1:30-31)*

Maria binti Sayuni,uliishi maisha yako kwa Upendo na matumaini kwamba ahadi za Mungu zitatimia.Maisha hayo yaliumba ndani yako moyo mkarimu kwa Bwana wa mabwana ambaye kwa hakika angekuja.Mama mpenzi wa Yesu na mama yangu,unaonyesha jinsi ninavyopaswa kuishi maisha yangu ya Kila siku Lakini bahati mbaya gani fundo hili....(taja fundo)limenipokonya uzuri wa Mungu,limeniondolea fadhila ya imani na matumaini Sasa kwa Uhuru nataka kuliwakilisha kwako Maria mfungua mafundo ili ulifungue na hivi niweze kuishi maisha ya hadhi ya Mkristo na mtoto wa Mungu.

**Maria mfungua mafundo, niombee mimi ninayekukimbilia**
**Sali mafungu mawili ya mwisho ya rozari.**

**Sali Sala inayopatikana katika Novena ya siku ya kwanza Sala hii inasaliwa Kila siku.**
**Kwa Maria mfungua mafundo**

**SIKU YA NNE**

**Sala ya utangulizi**
**Sali mafungu matatu ya Rozari**
**(Mafumbo ya siku husika**)

Somo la Biblia

*Mariamu akasema,tazama Mimi ni mjakazi wa Bwana na iwe kwangu Kama ulivyosema(Luk1:38)*
Ee Maria ulisadiki ujumbe wa malaika Gabriel na hivi akaruhusu mwendelezo wa Mungu kwa ubinadamu.Maria wewe ni wa kwanza na mfuasi mkamilifu kwa sababu ulisikiliza Neno la Mungu,ulipokea na kuliishi.Weqe NI kielelezo Cha wote wanaotaka kuwa wafuasi wa Yesu.
Kwa sababu ya utayari wako waisikia sauti ya Mungu,ukawa Mama wa Mungu.Fadhili gani umejaliwa,Ee mama mimi pia nasadiki Mungu na Neno lake.Nasadiki pia Yale ambayo mama Kanisa anafundisha lakini ninapungukiwa na uwezo wa kuyaishi kwa sababu ya fundo hili....(taja fundo) Ee Maria mfungua mafundo chukua fundo hili linalonifanya mfungwa wa mawazo yangu na vilema vyangu. Inakupa kwa sababu linanizuia kuishi maisha ya imani yenye kizaa matumda.

**Maria mfungua mafundo niombee mimi ninayekukimbilia**
**Sali mafungu mawili ya mwisho**
**Sali Sala ya mwisho Kwa Maria mfungua mafundo**

**SIKU YA TANO**

**Sala ya utangulizi**
**Sali mafungu matatu ya Rozari**
**(Mafumbo ya siku husika)**

Somo la Biblia

*Mariamu akaondoka siku hizo akaenda hata nchi ya milimani kwa haraka mpaka mji mmoja wa Yuda,akaingia nyumbani kwa Zakaria akamwambia Elizabeth.Ikawa Elizabeth aliposikia kule kuamkia kwake Mariamu,kitoto kichanga kikaruka ndani ya tumbo lake; Elizabeth akajazwa Roho Mtakatifu;akapaza sauti kwa nguvu akasema,"Umebarikiwa wewe katika wanawake,naye mzao wa tumbo lako amebarikiwa.Limenitokeaje neno hili hata mama wa Bwana. wangu anijilie Mimi?.Maana sauti ya kuamkia kwako ilipoingia masikioni mwangu, kitoto kichanga kikaruka kwa shangwe ndani ya tumbo langu.Naye heri aliyesadiki;kwa maana yatatimizwa aliyoambiwa na Bwana (Lk1:39-45*

Ee Maria mfungua mafundo, upendo wako hupita ufahamu wote.
Hujifikirii wewe mwenyewe ila namna ya kuleta Habari Njema kwa jirani,jamaa,rafiki na wahitaji....Huhitani kusema neno ila uwepo wako unasema maneno tele.Wewe niI kielelezo Cha wote wanaotaka kuwa wafuasi wa Yesu Kristo.Mimi pia Maria,ni mhitaji mkubwa,njoo nitembelee kama ulivyomtembelea Elizabeth,Ee Maria wa shauri jema.Ee Maria mama yangu mfungua mafundo.mlete Yesu katika maisha yangu.Ninaliweka fundo hili mikononi mwako.....(taja fundo) ulifungue Ee mama,na uniweke huru ili nikue katika upendo.

Maria mfungua mafundo niombee mimi ninayekukimbilia.

**Sali mafungu mawili ya mwisho ya rozari.**
**Sali Sala ya mwisho inayopatikana katika Novena ya siku ya kwanza**
**Kwa Maria mfungua mafundo**

**SIKU YA SITA**

**Sala ya utangulizi**
**Sali mafungu matatu ya Rozari**
**(Mafumbo ya siku husika)**

Somo la Biblia

*Naye Maria akasema"Moyo wangu wamwadhimisha Bwana,na roho yangu inamfurahia kwa sababu ya Mungu Mwokozi wangu.Kwa kuwa amemwangalia kwa huruma mtumishi wake mdogo, hivyo tangu Sasa vizazi vyote vitaniita mbarikiwa.Kwa kuwa Mwenyezi Mungu amenitendea makuu,jina lake ni Takatifu.Huruma yake kwa watu wanaomcha,hudumu kizazi hata kizazi.Amefanya mambo makuu kwa mkono wake;amewatawa ya wenye kiburi katika mawazo ya ya mioyo yao;amewashusha wenye vyeo kutoka viti vyao vya enzi,akawakweza wanyenyekevu.Wenye njaa amewashibisha mema matajiri amewaacha waende mikono mitupu (Lk1:46-53)*

Ee Maria Wewe ni shule na Mwalimu wetu.Unatufundisha kukiri ukuu wako wa . Mungu katika t yetu na pia wewe ni kielelezo Cha moyo wa shukrani.Mambo mangapi Mungu ametutendea na hatujaweza kusema Asante na katika mioyo yetu hatujajijengea tabia ya kumsifu na kumtukuza Mungu kwa uwepo wake kati yetu.Maria.Mwombezi wa neema zote umetuzawadia zawadi hii

Naliweka mikononi mwako fundo hili.......(taja fundo),linalonizuia kuona na kupokea uzuri wa Mungu katika maisha yangu.Ninalibadilisha na ile zawadi iliyo mikononi mwako,inayotoka kwa Bwana Mungu wangu.

Maria mfungua mafundo niombee mimi ninayekukimbilia

**Sali mafungu mawili ya mwisho Sali Sala ya mwisho inayopatikana katika Novena ya kwanza**
**Kwa Maria mfungua mafundo**

**SIKU YA SABA**

**Sala za utangulizi**
**Sali mafungu matatu ya Rozari**
**(Mafumbo ya siku husika)**

Somo la Biblia

*Ikawa baada ya siku tatu,walimkuta hekaluni,ameketi Kati ya walimu akiwasikiliza na kuwauliza maswali;nao wote waliomsikia walimu akiwasikiliza na kuwauliza maswali nao wote waliomsikia walistaajabia ufahamu wake na majibu yake.Walipomwona walishangaa,na mama yake akamwambia, Mwanangu,kwanini umetufanyia hivi?Tazama,baba yako na mimi tumekutafuta kwa huzuni." Naye akawaambia"kwanini kunitafuta?Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya baba yangu?"Lakini hawakuelewa neno alilowaambia.Akashuka pamoja nao,akafika Nazareth,na aliwatii;mama yake akayatunza maneno hayo yote moyoni mwake (Lk 2:46-51)*

Ee Maria, wewe ni kielelezo chetu Cha tafakari.Katika yote uliyopokea juu ya Yesu,hukuhoji Wala kutaka ufafanuzi lakini ulijifunza kuyaweka yote moyoni mwako.Chumba kilichofichika kinachofaa kwa tafakari na hakuna anayekijua au kukiona ila Mungu.Hekima gani unayo,Ee Maria.Kila akuonaye hukupa moyo mtulivu,matamu,yenye huruma na wazi.Mama wa hekima nisaidie kutafakari yote katika ukimya huku nikiongea na Bwana ninapokukabidhi yote yanayotokea katika maisha yangu, huku nikiyapokea Kama mapenzi ya Mungu.

Mikononi mwako naliweka fumbo hili.......(taja fundo)lililofanya maisha yangu kuwa magumu na ya kuumiza kwa miaka mingi.Sikiliza Sala yangu Maria mama wa shauri jema
**Maria mfungua mafundo niombee mimi ninayekukimbilia**
**Sali mafungu mawili ya mwisho ya rozari**
**Sali pia Sala ya mwisho kwenye novena ya kwanza**
**Kwa Maria mfungua mafundo**

**SIKU YA NANE**

**Sala ya utangulizi**
**Sala mafungu matatu ya Rozari**
**(Mafumbo ya siku husika)**

Somo la Biblia
*Siku ya tatu kulikuwa na harusi huko Kana,mji wa Galilaya;naye mama yake Yesu alikuwako.Yesu naye alikuwa amealikwa arusini pamoja na wanafunzi wake.Hata divai ilipokwisha,mama yake Yesu akamwambia"hawana divai"Yesu akamwambia,"mama nina nini nawe? Saa yangu haijawadia.Mama yake akamwambia watumishi"Lolote atakalowambia,fanyeni"(Yoh2:1-5)*

Nakimbilia ulinzi wako Ee Maria Mama yangu.Kwa huruma na upendo wako na kujali kwako tayari unaona magumu yanayopitia familia yangu.Unaona machozi mchana na usiku.Unaona mapambano yanayoonekana kuendelea bila mwisho.Lakini kama unavyoiombea pia na kusema"Lolote atakalowambia fanyeni".Iombee familia hii ambayo imechanwa chanwa. vipande kwa umasikini ulevi matatizo ya kimahusiano maombolezo upotevu na ukame wa kiroho na ifungue milango yake wazi ili Kristo aingie.Ili hili lifanyike,ninaweka katika mikono yako ya kimama fundo
.....(taja fundo)

Najua utalifungua na Kristo atachukua mahali pake stahiki katika familia hii.Sikiliza sala yangu Maria na uwe kielelezo changu na kiongozi wetu

Maria mfungua mafundo niombee mimi ninayekukimbilia

**Sali mafungu mawili ya mwisho**
**Sala ya mwisho kwenye novena ya siku ya kwanza.**
**Kwa Maria mfungua mafundo**

**SIKU YA TISA**

**Sala ya utangulizi**
**Sali mafungu matatu ya Rozari**
**(Mafumbo ya siku husika)**

Somo la Biblia

*Penye Msalaba wake Yesu walikuwa wamesimama na mamaye,na umbu la mamaye, Mariamu wa Kleopa,na Mariamu Magdalena.Basi Yesu alipomwona mama yake,na yule mwanafunzi aliyempenda amesimama karibu,alimwambia mama yake,"Mama,tazama,mwanao".Kisha akamwambia yule mwanafunzi,"Tazama,mama yako".Tangu saa ile mwanafunzi yule akamchukua nyumbani kwake (Yoh 19:25-37)*

Ee Maria, maisha yetu ya. kiroho yalitoka kwako Maria wewe ni mzizi unaobeba au,wewe ni mama unayetoa tunda takatifu la tumbo lako,wewe ni pambazuko unayelitangaza jua,

Ulipo wewe Yesu yupo pia.Kukupa wewe ni kumpata mwanao Kristo Yesu,Kupitia kwako ni njia fupi na ya uhakika, Mkombozi wangu amenipa wewe uwe mama yangu.Kama mtume Yohana nataka kukuchukua nyumbani kwangu, Kutoka ndani kabisa ya moyo wangu nijifunze kupatanisha maisha yangu na Kristo,Hapa na sasa hivi nakiri pingamizi langu na mikononi mwako,Ee Malkia wa huruma naweka fundo hili (taja fundo)ili niweze kusikiliza na kuishi anachoniambia Kristo.

Maria mfungua mafundo niombee mimi ninayekukimbilia

**Sali mafungu mawili ya mwisho**
**Sala ya mwisho inayopatikana katika Novena ya siku ya kwanza**
**Kwa Maria mfungua mafundo.**

**SALA YA SHUKRANI KWA BIKIRA MARIA MFUNGUA MAFUNDO**

Kwa moyo ulijaa shukrani nakuja kwako Maria mfungua mafundo mama na Malkia wangu.Asante kwa kunikaribisha mimi Mtoto katika nyumba yako,ili uweze kufungua mkanda wa maisha yangu uliyojifunga.

Asante kwa kuchukua mzigo,maumivu, huzuni na mashaka yangu niliyokuwa nikibeba katika maisha yangu.Sasa naweza kuipata tena ile furaha ya mtoto wa Mungu.

Asante kwa kutoelemewa na uzito wa mafundo katika maisha yangu, lakini Kama mama wa shauri jema ulinipokea Kama mwanampotevu ili uweze kunijalia maisha mapya.

Asante kwa kunikaribisha katika shule ya Yesu,ambamo wewe ni Mwalimu na Malkia na daima wanikumbusha kufanya kama Yesu anavyoniambia kufanya,ili nibaki  nimeungana naye aliye chemichemi ya furaha na maisha ya daima.

Asante kwa kwa kunisimamia upande wangu na kunifundisha kunipenda na kufanya kile tu kinachompendeza Mungu Baba yangu,ili niweze kushiriki katika mpango wake wa milele alioniwekea tangu mwanzo.